**SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR**

# TANGAZO LA USAJILI WA WAKALA WA KUUZA TIKETI ZA MELI YA MV MAPINDUZI II

Shirika la Meli Zanzibar linatangaza fursa ya biashara ya kuuza tiketi za MV Mapinduzi II. Jiunge na mtandao wetu wa usafiri wa baharini leo!

---




**MV Mapinduzi II**

**Taarifa Kuu:**

Shirika la Meli Zanzibar, inakaribisha Kampuni zenye nia na uwezo kujiunga na mtandao wetu wa wakala wa kuuza tiketi kwa ajili ya Meli ya MV Mapinduzi II kwa kuwa na sifa zifuatazo.

**Sifa za Kampuni:**

1. **Usajili wa Kampuni:**
    - Kuwa na cheti cha usajili biashara (BPRA) chenye uhalali.
    - Kuwa na ofisi/kituo cha kudumu kinachofikiwa kwa urahisi na wateja.
    - Awe na uwezo wa kuhifadhi malipo kwa tiketi zilizouzwa.
    - Kampuni inatakiwa kuambatanisha nakla ya cheti cha Mlipa kodi.
    - Kampuni inatakiwa isajiliwe na Mamlaka ya Usafirishaji Baharini Zanzibar. (ZMA)
    - Kampuni iwasilishe uzoefu wake wa angalau mikataba miwili ya Uwakala kwa kazi ya uuzaji wa Tiketi.
2. **Uwezo wa Kifedha:**
    - Kuwa na mtaji wa kutosha wa kuanzisha na kuendesha kituo cha tiketi.
    - Awe tayari kulipa ada ya udhamini na kufanya malipo ya awali kwa tiketi.
3. **Uzoefu na Sifa Binafsi:**
    - Upendeleo utawekwa kwa wale walio na uzoefu katika uuzaji wa tiketi za usafiri baharini na huduma za wateja.
    - Uwezo wa kufanya kazi kwa usahihi na haraka katika mfumo wa kompyuta.
    - Tabia nzuri na uaminifu mkubwa.
4. **Kiwango cha Kamisheni:**
    - Muombaji ainishe kwa barua kiwango cha Kamisheni atakachohitaji kwa kila tiketi atakayouza.

**Faida za Kuwa Wakala Wetu:**

- **Mapato Thabiti:** Utapata Kamisheni ya kiasi cha asilimia ya kila tiketi unayouza.
- **Matumizi ya Jina:** Ruksa ya kutumia jina la kampuni na alama ya biashara yetu katika uuzaji.
- **Mafunzo ya Kutosha:** Utapokea mafunzo kamili kuhusu mfumo wa uuzaji wa tiketi na huduma kwa wateja.
- **Usaidizi wa Kiufundi:** Timu yetu itakuwa tayari kukusaidia kiufundi na kibiashara kila wakati.
- **Nyongeza ya Wateja:** Utapata wateja kwa kiasi kikubwa kutokana na umaarufu wa Meli yetu.

**Jinsi ya Kuomba:**

- Muombaji anatakiwa awasilishe maombi yake kwa barua kwa kumuandikia Mkurugenzi Muendeshaji Shirika la Meli Zanzibar.

- Muombaji awasilishe maombi hayo yakiwa kwenye bahasha iliyofungwa vizuri kwa kuainisha aina ya kazi aliyoiomba.

Anuani ya Barua:

**Mkurugenzi Muendeshaji,**

**Shirika la Meli Zanzibar,**

**S.LP. 80.**

**Zanzibar.**

Maombi hayo ya wasilishwe si zaidi ya Ijumaa tarehe 17/02/2026.

**Mawasiliano:**
Ikiwa una sifa za kujiunga na timu yetu, tafadhali tuma maombi yako kwa:

**Barua Pepe:** [info@shipco.go.tz]
**Kichwa cha barua: MWOMBAJI WAKALA TIKETI - MV MAPINDUZI II**
**Muhusika:** [Idara ya Masoko, Utafiti na Masoko]

---

**Shirika la Meli Zanzibar**
"*Tunajivunia kuhudumia wateja wetu kwa usalama.*"